

CHAPISHO LA KWELI
MUONGOZO WA REDIO

MUONGOZO WA UKATAJI MITI, UHARIBIFU WA MISITU, NA JUHUDI ZA UREJESHAJI MISITU

TANZANIA

UTANGULIZI

Ukataji miti na juhudi za urejeshaji wa misitu ina uhusiano muhimu uliounganishwa inapofikia suala la mazingira na afya ya sayari yetu. Ukataji miti ni uondoaji wa miti na misitu ili kutengeneza nafasi na kuwezesha matumizi mengine tofauti ya ardhi hiyo. Mara nyingi, ukataji miti huchangiwa na kilimo na mahitaji ya ardhi zaidi ya kukuza mazao na biashara. Ukataji wa miti pia hufanywa ili miti hiyo itumike kwa ujenzi au kama mali ya kibiashara na uuzaji – (wakati mwingine kinyume cha sheria), au kwa matumizi ya mbao na kuni. Ukataji miti ni shida kubwa ya mazingira kwa sababu inaleta tishio kwa afya ya sayari. Wakati misitu hukatwa au kuteketezwa, kuna upotezaji mkubwa wa wanyamapori,uharibifu wa mifumo ya ikolojia, jamii, na pia riziki kwa watu wanaofanya kazi katika viwanja vya utalii. Shida moja kubwa zaidi ukataji wa miti husababisha kuongezeka kwa kiwango cha gesi chafu angani (kaboni dioksidi). Kwa sababu miti kawaida hunyonya gesi hiyo chafu ya kaboni dioksidi (CO2) kupitia njia ya 'photosynthesis,' ambayo ni mchakato wao wa asili wa uundaji wa nishati, miti hupunguza kiwango cha CO2 angani kwa kiwango kikubwa. Misitu inapoharibiwa na kuteketezwa, kwa mfano, kwa madhumuni/matumizi ya kilimo, gesi chafu ya kaboni dioksidi huzalishwa na kuchangia kwa ongezeka la kiwango cha joto duniani. Na hapa ndipo suala la upandaji miti linaingia. Upandaji miti ni upandaji misitu wa makusudi, na kukuza misitu kama njia ya kupambana na ongezeko la kiwango cha joto duniani, pamoja na athari zingine zote mbaya ambazo zinaweza kutokea. Jitihada za upandaji miti sio tu kwa ajili ya urejeshaji wa misitu, lakini pia inajumuisha utengenezaji wa sera, mipango ya serikali, na mikakati kamili/ madhubuti ambazo zote zinatengeneza ardhi, na vile vile kuleta suluhisho la ulinzi wa misitu katika siku zijazo.

TAFSIRI

Kinyonya kaboni (carbon sink) ni kitu chochote kinachoweza kuchukua na kuhifadhi gesi chafu ya kaboni dioksidi. "Carbon sink" zina jukumu kubwa katika kulinda na kudhibiti mazingira, na mifano ya hizi "carbon sink" kubwa ni kama vile bahari za dunia, mimea (ikijumuisha misitu), na udongo.

Uhifadhi ni zoea la kulinda maliasili ili iweze kuendelea vyema na kufikia vizazi vijavyo pia. Mbinu za uhifadhi bora ni jambo muhimu katika masuala ya mazingira

Ukataji miti ni uondoaji wa makusudi wa miti na misitu. Mara nyingi hufanywa ili kutoa nafasi kwa kilimo. Ukataji wa miti na uharibifu wa misitu umeharakishwa na shughuli za kibinadamu tangu mwaka wa 1960. Na ingawajiinaweza kutoa nafasi ya kazi na upanuzi wa kilimo, imeathiri vibaya mazingira ya asili, bioanuwai, na kuleta mabadiliko ya tabia nchi.

Kuzorota kwa ardhi ni upotevu au

madhara kwa virutubisho na ubora wa udongo katika mazingira yoyote. Kuzorota kwa ardhi kunatishia mazingira katika suala la mabadiliko ya tabia nchi, na vile vile kusababisha uhaba wa chakula na kuwa na ardhi inayozalisha mazao na dawa inayotosha.

Urejeshaji wa misitu ni upandaji wa makusudi wa miti na misitu ambayo imeharibiwa na kumalizwa, kwa kawaida kupitia kwa ukataji wa miti.

Umuhimu wa misitu (WWF):
Msitu huwa na matumizi kadhaa ya muhimu, ikiwa ni pamoja na:

Kutega Gesi Chafu (GreenHouse Gases) na Kuzuia Mabadiliko ya tabia nchi

Misitu ina jukumu muhimu sana katika kudhibiti hewa tunayopumua na kulinda dunia kutokana na miale ya joto ya jua. Dioksidi ya kaboni inachukuliwa kama gesi chafu, ambayo ni gesi hatari kwa anga na inaharakisha mabadiliko ya tabia nchi na ongezeko la kiwango cha joto duniani. Miti hutumia gesi chafu ya dioksidi kaboni kwa mchakato wao wa kuunda nishati, na kwa hivyo hupunguza na kudhibiti aina hii ya gesi angani.

Kuwa makao ya wanyamapori na bioanuwai (biodiversity)

Misitu ni nyumba ya mamia ya maelfu ya wanyama na viumbe vya kipekee. Upotezaji wa wanyamapori huathiri mazingira asili, ambapo upotezaji wa aina moja ya mmea au mnyama huweza kuathiri mazingira jirani vibaya. Kwa mfano, mnyama wa aina moja anaweza kuongezeka idadi kwa sababu mnyama mwingine anayewinda na kumla ili kudhibiti idadi hii amepunguzwa kwa sababu ya ukataji wa miti, uharibifu wa misitu unaosababisha wanyama wasiweze kuishi ipasavyo.

Kutoa chakula, mimea ya dawa, na vyanzo muhimu vya maisha

Misitu sio tu makazi ya bioanuwai, lakini pia kwa binadamu ambao wameishi ndani na karibu ya misitu kwa vizazi na karne nyingi. Kwa hivyo, upotezaji wa misitu unaweza kusababisha upotezaji wa ajira kama utafiti kuhusu dawa au upotezaji wa makao, na hivyo pia kupoteza ule utamaduni na historia ya watu wa asili katika maeneo fulani na misitu.

UKATAJI MITI NA UREJESHAJI WA MISITU ULIMWENGUNI:

Ukataji wa Miti na Uharibifu wa Misitu Ulimwenguni:
Inakadiriwa kuwa kila mwaka, ulimwengu hupoteza takriban kati ya hekta milioni 5 na milioni 10 za misitu, na ukataji miti mwingi ulimwenguni hufanyikia eneo la Amerika Kusini. Kwa upande mwingine, hekta milioni 5 inakaribiana kidogo na ukubwa wa nchi ya Togo, na hekta milioni 10 za ardhi inakaribiana kidogo na nchi ya Liberia. Kulingana na Shirika la Wanyamapori Duniani (WWF), maeneo kadhaa makubwa ya ukataji miti ni katika msitu wa mvua wa Amazon ulio nchini Brazil, na misitu mingine Afrika ya Magharibi, ikiwa ni pamoja na kisiwa cha Madagascar. Ukataji miti mingi katika maeneo haya unasukumwa na mahitaji ya ardhi kwa matumizi ya kilimo. Hata hivyo, misitu pia hukatwa kwa ajili ya uuzaji wa mbao na ujenzi/utengenezaji wa mali za kibiashara. Kwa ujumla, kiwango cha ukataji miti ulimwenguni ni 0.5 %.

Urejeshaji misitu ulimwenguni kote:
Jitihada za upandaji miti ili kurejesha misitu ulimwenguni kote zimeonekana kama miradi mikubwa ya upandaji miti na ushirikiano na sera za serikali na pia taasisi zisizo za kiserikali. World Economic Forum (WEF) mnamo 2020 ilizindua mpango wa kuendesha upandaji wa miti trilioni moja ulimwenguni. Mpango huu umeungwa mkono na kupitishwa katika nchi kadhaa ulimwenguni. Mashirika kama Taasisi ya Wanyamapori Duniani, Jiografia ya Kitaifa, Benki ya Dunia, na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) hufanya kazi ya kufanya utafiti na kuunda mipango ya kufanya kazi kwa maisha endelevu na yenye afya hasa linapokuja suala la misitu yetu.

UKATAJI MITI BARANI AFRIKA:

Wakati mwingine misitu huitwa “Mapafu ya Afrika.” Misitu barani kote Afrika hutenda jukumu muhimu katika afya ya mazingira na ya jamii, na pia kwa uchumi wa mataifa mengi. Kinachochochea ukataji miti katika bara la Afrika mara nyingi ni kilimo - ambapo misitu hupunguzwa na kuteketezwa ili kutoa nafasi na ardhi zaidi ya kupanda mimea. Lakini, ukataji miti na uharibifu wa misitu pia hufanyika kwasababu ya kuzalisha mkaa ya kupikia na uuzaji, na kwa kupata mbao. Ingawa kilimo kinaweza kutoa ajira zaidi kwa jamii, mahitaji ya ardhi ya kukuza na kuuza chakula inaweza kuwa na athari mbaya kwa bara lote, ikiwa ni pamoja na:

- Ukosefu wa misitu ya kudhibiti gesi chafu, na uzalishaji wa kaboni kutokana na kuteketeza misitu
- Mmomonyoko wa ardhi kutokana na kilimo duni (ulimaji zaidi wa ardhi)
- Uharibifu wa makazi ya kipekee na bioanuwai
- Tishio kwa jamii za wenyeji ambao wanaishi na kufanya kazi zao katika misitu ya asili

Kuzingatia mazoea endelevu barani Afrika

Mikakati kama mpango wa Ushirikiano wa Misitu ya Kitropikali 2020 (Tropical Forest Alliance, TFA2020) na Mpango wa Mafuta ya Palm (Africa Palm Oil Initiative, APOI) yote yanahimiza serikali na sekta binafsi kutafuta njia bora za kulima katika ardhi na kuunda mauzo ya nje bila kutumia mbinu zinazodhulumu haki za wakulima au mshahara wao, au kusababisha unyonyaji na matumizi ya ardhi kwa kiwango kikubwa zaidi ya inavyostahili. Malengo TFA2020 ni kuunda minyororo ya ugavi ya bidhaa ambazo hazileti uharibifu wa miti na misitu, kama mawese (palm oil), nyama ya ng'ombe, soya na makaratasi. Usambazaji kupitia kuleta pamoja sekta mbalimbali za binafsi, mashirika na serikali za kitaifa ili kusimamia usambazaji, bei, mnyororo na kutengeneza mazingira ya kilimo cha usawa. Sawa na TFA, Mpango wa Afrika wa Mafuta ya Palm unakusudia kuunda aina ya mbinu endelevu za kilimo na utengenezaji wa mafuta ya mawese, na kuepuka kilimo cha zaidi katika nchi kumi zinazozalisha mafuta hayo ya mawese.

- **Ya ziada kuhusu TFA yanapatikana hapa: https://www.tropicalforestalliance.org/**
- **Ya zaida kuhusu APOI yanapatikana hapa: https://bit.ly/3d4iZ8m**

ATHARI ZA UKATAJI MITI NA UREJESHAJI WA MISITU:

UKATAJI MITI

Mabadiliko ya tabia nchi

Kwa sababu miti na misitu huhifadhi gesi chafu ya kaboni dioksidi, na vile vile huhifadhi wanyamapori wengi muhimu na pia anuwai, ni sehemu muhimu katika afya ya sayari. Kuzuia mabadiliko ya tabia nchi kunahusishwa na kuhifadhi misitu, miti na udongo ulimwenguni kote.

Upotezaji wa wanyamapori, bioanuwai, na tiba

Misitu mikubwa ni makao ya aina kadhaa za wanyama, bioanuwai, na mifumo ya ikolojia. Kupotea kwa aina hizi za mazingira asili kunaweza kuathiri jamii zinazozunguka, na pia utenda kazi wa mazingira kwa jumla. Wanyamapori pia wana jukumu katika hewa bora, udongo na udhibiti wa mazingira. Mwisho, misitu ni makao ya viungo vingi vya madawa, ambazo anuwai na binadamu wanategemea sana. Kuharibiwa kwa misitu kunaweza kuwa na athari mbaya kwa uzalishaji wa dawa hizi, na vile vile kwa utafiti wa dawa mpya za kupambana na magonjwa kama ya saratani au VVU.

Upotezaji kiuchumi au unyonyaji wa mapato ya kukimu maisha

Kwa muda mfupi, kukata miti kwa ajili ya mradi ya kilimo kunaweza kuonekana kama fursa inayoleta ajira. Lakini, ikiwa miradi ya kilimo haifanywi kwa mbinu endelevu, ambayo ndivyo ilivyo kawaida, inaweza kusababisha uharibifu wa ardhi kwa muda mrefu na umaskini wa jamii za kitamaduni ambazo zilitegemea msitu ili kujikimu kimaisha.

UREJESHAJI WA MISITU

Kurejesha bioanuwai

Misitu ni makao ya zaidi ya 80% ya

viumbe hai duniani, na juhudi za upandaji miti husaidia kurejesha na kulinda wanyama na majukumu yao muhimu katika misitu yetu.

Kukomesha (na kurejesha) mmomonyoko wa udongo

Kwa sababu miti inalinda udongo kutokana na upepo na mvua, udongo uko katika hatari kubwa ya kumomonyoka, ambayo inaweza kusababisha hali mbaya kwa kilimo na mafuriko ya ghafla. Upandaji miti tena unaweza kubadilisha hali hii na kusaidia mfumo wa ikolojia ambao unaweza kujilinda na kujidhibiti yenyewe na virutubisho vyake.

Kudhibiti na kupunguza kiwango cha gesi chafu ya kaboni dioksidi hewani

Misitu na bahari hunyonya kaboni, na husaidia kudhibiti kiwango cha gesi hatari katika anga na kutuwezesha kuishi na kupumua vizuri duniani. Upandaji miti ni muhimu sana kwa afya ya sayari yetu.

Kuleta ajira katika sera na kilimo endelevu, ujenzi, na biashara

Miradi ya upandaji miti pamoja na sera zinazolenga mazingira zina uwezo wa kutengeneza nafasi za ajira na kuchangia kiuchumi katika jamii, na ambazo zitadumu kwa muda mrefu, bila kutawaliwa na shinikizo la kuzalisha kiasi kikubwa cha aina moja ya mmea au bidhaa. Kwa muda mrefu, misitu zaidi na masoko yaliyodhibitiwa ambayo yanalenga mazingira na sera, zinalinda dunia na vile vile kuzuia unyonyaji na ukosefu wa usalama kwa binadamu.

Ulinzi wa ardhi

Kujitolea kwa jamii yoyote au nchi katika upandaji miti inaweza kulinda ardhi, kwa kuteua maeneo fulani yatakayopandwa tena, na vile vile kuteua ulinzi wa misitu iliyopo na ardhi kutokana na kubomolewa au kuuzwa kwa madhumuni mengine.

ATHARI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII ZA UKATAJI MITI NA UHARIBIFU WA MISITU

Ukataji miti na uharibifu wa misitu unaweza kushinikizwa na hali ya umaskini, au hitaji la kutafuta mapato linaweza kusababisha ukataji miti, kwani watu zaidi wanahitaji fursa za kazi. Ni jambo la dharura basi kutafuta njia endelevu za kilimo, pamoja na mifumo ya kushughulikia sababu kuu za umaskini na madhata yaliyowachwa kufuatia kipindi cha ukoloni hadi sasa, katika mataifa mengi ya Afrika.

Ukataji miti na uharibifu huathiri bei za chakula, usafirishaji wa bidhaa, maendeleo na gharama za dawa, na pia mengi zaidi. Mara nyingi hii huwa ni kwa njia hasi sana. Jitihada za upandaji miti na uhifadhi wa misitu zinaweza kudhibiti vitu hivi, na vile vile kuunda njia bora za siku za usoni, ili vizazi vijavyo viwe na ulimwengu mzuri wa kurithi.

Kwa sababu ukataji miti unatishia maarifa asilia, utamaduni, na pia lugha, kuna uharaka wa kutetea misitu yetu kwa sababu za kitamaduni pamoja na mazingira na uchumi.

ONDOA HADITHI POTOFU (UZUSHI), PATA UKWELI

UZUSHI	UKWELI
Ukataji wa misitu hauniathiri mimi	Ukataji wa misitu huathiri kila mtu, kwani unasababisha ongezeko la kiwango cha joto kote duniani. Ukataji miti huathiri jamii na afya kwa jumla, ambayo pia moja kwa moja huathiri ulimwengu wa baadaye na vijana watakaourithi.
Upanda miti ili kujaribu kurejesha misitu hukanusha/kubadilisha (reverse) ule uharibifu wa misitu	La kusikitisha ni kwamba juhudi za upandaji miti ili kurejesha misitu haibadili/kukanusha kabisa zile athari za ukataji miti - bioanuwai ni ngumu sana kurudia, na wakati aina za vumbe hai hasa wanyamapori zinapotea huwezi kuwafufua. Uhifadhi ni muhimu kulinda hizo. Lakini, upandaji miti ni muhimu sana kulingana na mabadiliko ya tabia nchi, kwani uwezo wa miti kuhifadhi gesi chafu ya kaboni ni njia moja ya kuchukua hatua kuhusu ongezeko la kiwango cha joto duniani.
Ukataji miti ni suala la mazingira tu	Ukataji miti na uharibifu wa misitu huathiri karibu sekta zote za maisha, kwa mfano katika uchumi. Mara nyingi inasahaulika kwamba uchumi unategemea rasilimali asili, na mifumo ya ikolojia inayofanya kazi. Ukweli huu hujitokeza mara tu mifumo ya asili inapoisha au kuharibiwa na shughuli za kiuchumi zilizounganishwa na hivyo kuzorota na asili kuacha kutoa huduma zile zake ambazo ziliweza kufanywa awali, bure. Huwezi kuendesha biashara ya uvuvi ikiwa mto utakauka, au ikiwa samaki hawapatikani mtoni tena. Haya ni sawa pia na uharibifu wa misitu na ongezeko la kiwango cha joto duniani. Mambo mengi ya maisha ya kila siku tunayoyachukulia kuwa ya kawaida katika masuala yetu ya maisha duniani yanaendelea kubadilika na sote tutaathiriwa.
Hakuna kitu chochote ambacho vijana wanaweza kufanya ili kusaidia kukomesha ukataji miti na uharibifu wa misitu.	Katika bara lote la Afrika, kuna harakati kubwa zinazoongozwa na vijana, kama harakati ya “Rise Up Movement,” ambayo ilianzishwa na mwanaharakati kijana wa Uganda, Vanessa Nakate kusaidia, ili kukuza sauti za wanaharakati kutoka barani kote. Kupitia harakati hii kubwa, vijana wanaweza kupata kazi na fursa za kujifunza kutoka kwa miradi au maslahi ya kila mmoja na hata pia kuweza kushirikiana. Harakati hii ya “Rise Up Movement” inaendeshwa katika nchi kadhaa, zikiwemo Uganda, Kenya, Somalia, Nigeria, Malawi, Togo, Zambia, Senegal, na Afrika Kusini.

JE, WAJUA? (ZA KIMATAIFA)

Afrika inahifadhi ya eneo la msitu la pili kwa ukubwa duniani kote. Ndani yake, kuna msitu wa mvua wa pili kwa ukubwa ulimwenguni kote, uliopo **katika Bonde la Kongo**, Afrika ya Kati - msitu ambao unapita katika nchi 6 za Afrika ya kati.

Zaidi ya 30% ya misitu ya ulimwengu wote inaaminika kuwa imeharibiwa, na uharibifu mwingi unaaminika kuwa umefanyika katika kipindi cha miaka 45 iliyopita.

(World Bank)

Zaidi ya watu bilioni 2 wanategemea misitu. Misitu hutoa makao, maisha, maji, na chakula. Kila kitu kutoka kwa matunda na mboga, dawa, vipodozi, karatasi, na sabuni hutoka misituni.

(UN)

Ingawa Afrika kwa sasa inachangia kiasi kidogo tu cha gesi chafu za ulimwengu wote, chanzo kikuu cha uzalishaji wa gesi chafu za barani ni ukataji miti na uharibifu wa misitu.

(World Bank)

Udongo unaweza kukosa virutubisho. Kukata au kuchoma msitu ili kupata ardhi ya kulima wakati mwingine huwa suluhisho la muda mfupi tu kwa kilimo. Mara nyingi ikiwa ardhi haipumzishwi, au kutumiwa kwa ukulima wa mbinu endelevu, udongo unaweza kunyonywa virutubisho vyote, na kusababisha mazao ya baadaye yasimee. Wakati hii inapotokea, ukataji zaidi wa miti na uharibifu wa misitu unaweza kutokea. Jitihada za upandaji miti na kurejesha misitu tena zinalenga kutekeleza kilimo endelevu na bei za soko ili kuepusha shinikizo kwa wakulima za kuzalisha kupita kiwango kinachostahili na kuendeleza kilimo duni.

JE, WAJUA? (TANZANIA)

Upanuzi wa kilimo, haswa uondoaji mkubwa wa miti ili kupata nafasi ya ardhi kwa kilimo cha mazao ya biashara kama pamba na tumbaku ni mojawapo ya sababu kuu za ukataji miti na uharibifu wa misitu nchini Tanzania.

Uharibifu wa misitu nchini Tanzania pia unatokana na uzalishaji wa mkaa na kuni.



Marafiki wa 'Jumuiya ya Usambara,' taasisi lisilo la kiserikali lenye makao yake nchini Tanzania, liliahidi kufadhili upandaji wa miti 500,000.



Kati ya miaka ya 1990 na 2010, Tanzania ilipoteza 19.4% ya maeneo yake ya misitu - au takriban hekta milioni 8 za msitu.



MFANO (UCHUNGUZI KIFANI):

Kupanda miti milioni 5 nchini Ethiopia

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, nchi ya Ethiopia imepoteza takriban 97% ya misitu yao kutokana na ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya kilimo. Kwa hivyo mnamo 2019, mradi uitwao “The Green Legacy” ulizinduliwa ili kujitolea kupanda miche ya miti milioni 5 katika juhudi za kurejesha hekta milioni 15 za misitu iliyokuwa imekatwa - hiyo ikiwa miti bilioni 20 ifikapo mwaka wa 2025.

Miche hiyo ya miti ilipandwa katika maeneo 38,000 kote nchini, na imefanywa tokea mwaka wa 2020 na pia 2021, ikiwa na matokeo mazuri kwa miti mingi iliyopandwa. Mradi huo umewezeshwa kupitia ushiriki wa vijana pamoja na wanajamii wazee, na watu wanaofanya kazi katika sekta ya mazingira.

Miradi kama wa “Green Legacy” hutuonyesha kwamba kuna uwezekano na pia hatua ili kupambana na ukataji miti na uharibifu wa misitu, na pia juhudi zinaweza kufanywa kwa njia kubwa, ikiwa ni pamoja na kwa kupitia ushiriki na uongozi wa vijana.

Pata taarifa kamili hapa: https://bit.ly/3vaiTUB

UPAZAJI SAUTI WA VIJANA (SAUTI ZA WANAHARAKATI VIJANA)

Afrika Kusini

Ayakha Melithafa ni mwanafunzi wa miaka 17 kutoka mtaa wa Khayelitsha (mjini Cape Town, Afrika Kusini) ambaye kupitia masomo yake ya mazingira amezungumza katika maeneo kama UN kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na vijana wengine ambao pia ni wanaharakati. Ayakha ni mwanafunzi katika Kituo cha Sayansi na Teknolojia huko Khayelitsha, na pia ni afisa wa uajiri na msemaji wa Muungano wa Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Afrika (African Climate Alliance) - kikundi cha utetezi wa mabadiliko ya tabia nchi kinachoongozwa na vijana. Kuanzia hapa, yeye na vijana wengine 15 hivi karibuni waliwasilisha malalamiko ya msingi kwa Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watoto (UN Committee on the Rights of the Child).

Kutoka kwa machangio wake kwa ombi la kisheria, Ayakha alibaini kuwa ukame wa Cape Town wa 2018 au “Day Zero” ilionyesha hitaji lililopo la kulindwa kwa mazingira na mifumo ya usimamizi wa rasilimali ambazo zinalinda afya ya sayari na wanadamu.

Harakati za Ayakha zinazingatia kuwawezesha vijana kujifunza kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na kuunda suluhisho, ili kuweka mazingira katika hali yenye afya.

Maelezo zaidi ya wanaharakati vijana wa Kiafrika yanaweza kupatikana hapa:: https://bit.ly/3bzLkn6

RASILIMALI

- WWF
- Our World in Data : Deforestation
- FAO as a part of the UN
- UN Africa Renewal
- National Geographic
- African Wildlife Foundation

MUONGOZO WA UKATAJI MITI, UHARIBIFU WA MISITU, NA JUHUDI ZA UREJESHAJI MISITU

MUONGOZO WA REDIO

MADA MAHUSUSI

"NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU UKATAJI MITI NA UREJESHAJI WA MISITU"

- Ukataji miti na uharibifu wa misitu ni nini? Kwa nini ni muhimu kuzungumza kuhusu?
- Ni kwa njia ipi ambayo ukataji miti huathiri jamii yetu?
- Ukataji miti utawaathirije vijana?
- Ni masuala yapi ya kawaida yanayopatikana katika jamii yako, kama matokeo ya ukataji miti na uharibifu wa misitu?
- Ni mambo gani unayoweza kuyafanya ili kusaidia kushughulikia masuala yanayohusiana na ukataji miti na uharibifu wa misitu katika jamii yako?

CHAGUA MADA (KUTOKA KWENYE ORODHA ILIYOPO)

"Ukataji miti na uharibiru wa misitu, na urejeshaji wa misitu ni nini? Na kwanini ni muhimu kuizungumzia, kuhusianisha na tabia za vijana?"

NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU (TAJA JINA LA MADA ULIYOICHAGUA) KWA MFANO: "UKATAJI MITI NA UPANDAJI MITI NI NINI?

- Kwa nini ni muhimu kuizungumzia kuhusianisha na tabia za vijana ? "
- Nini umuhimu wa misitu?
- Kuna uhusiano gani kati ya misitu na maarifa asilia?

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO

SAUTI ZA UMMA

Lengo la sauti za umma
Kupata maoni mengi kuhusu mada moja

Utazungumza na nani?
Mtu yeyote kutoka kwa jamii.

Swali
Je, unajua uharibifu wa misitu ni nini? Au unajua ni kwanini miti ni muhimu kwa mazingira?

MAONI YA SAUTI

Lengo la maoni ya sauti
Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanaijali.

Utazungumza na nani?

- Mtu anayehusika katika mradi wa upandaji miti.
- Shirika la kijamii ambalo linashiriki katika harakati za mabadiliko ya tabia nchi.
- Mwanajamii anawajibika kwa upandaji miti na kurejesha misitu tena.

Muongozo wa mazungumzo:

- Kwa nini misitu ni ya muhimu?
- Miti inalindaje afya zetu na afya ya sayari?
- Ni njia gani ambazo watu wanaweza kushiriki ili wasaidie kuhifadhi misitu?
- Kwanini kilimo na ardhi zinapaswa kudhibitiwa?
- Kwa nini watu wanapaswa kujua na kujali kuhusu ukataji miti na uharibifu wa misitu?

TANGAZO LA UMMA (PSA)

Lengo la Tangazo la Umma
Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

Unda tangazo la umma (PSA) inayoamsha mwamko kuhusu umuhimu wa kuzungumza na vijana kuhusu (mada inayohusiana na ukataji miti/urejeshaji wamisitu).

Sauti 1: Asha, je, wajua Afrika ina msitu wa pili mkubwa duniani kote? Na pia msitu huo unakabiliwa na tishio la uharibifu kupitia ukataji miti kwa ajili ya kilimo au biashara, au hata wakati mwingine uuzaji haramu wa kuni/mbao?

Sauti 2: Sikujua hayo! Miti na misitu ni muhimu sana kwa uchumi wetu, dawa, utamaduni, na hewa tunayopumua!

Sauti 1: Ndio! Na inaonyesha jinsi ilivyo muhimu kuilinda misitu yetu na kuhakikisha kwamba inatunzwa, ili nasi tuweze kujitunza wenyewe.

Sauti 2: Kweli kabisa!

Wito (kauli mbiu): Okoa miti - ni mapafu yetu!

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa sauti:
Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

Utazungumza na nani?

- Kijana anayehusika katika mradi wa upandaji miti.
- Mtaalamu ambaye anahusika katika mradi wa upandaji miti.

MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kuunda kipindi chako.

[MWANZO/KUFUNGUA KIPINDI:]
Mtangazaji 1: Imetimia [TAJA SAA]. Karibu ujiunge nasi kwenye makala ya [TAJA JINA LA KIPINDI] hapa [TAJA JINA LA STESHENI] . Mimi ni [TAJA JINA LAKO]

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO]. Kwenye Makala yetu ya leo, tutazungumza kuhusu ukataji miti na urejeshaji wa misitu.

Mtangazaji 1: Lo! Hiyo inaonekana itakuwa mada kubwa! Tutaanzia wapi?

Mtangazaji 2: Si tuanze kwa kutafsiri mada yetu?

Mtangazaji 1: Haya basi, twende kazi!

Mtangazaji 2: Ukataji miti ni mchakato wa kusafisha misitu ili iwe inaweza kutumika vingine, kwa mfano ardhi hiyo itumike kwa kilimo. Urejeshaji wa misitu tena nayo ni kinyume chake, na inaweza kutimizwa kwa kupanda miti tena na kulinda misitu iliyopo kutokana na uharibifu zaidi.

Mtangazaji 1: Kwa hivyo, uharibifu wa misitu na wanyama pori. Suluhisho ya mambo haya yote yanaweza kusaidia kuijenga upya mifumo ya mazingira na kuzuia ueneaji wa uharibifu zaidi.

Mtangazaji 2: Naam, hiyo ni kweli! Na haya yote ni sehemu ya haki za kimazingira (environmental justice)!

Mtangazaji 1: Ni vizuri kujua hayo. Kwa hivyo ukataji miti (yaani uharibifu wa misitu) pia inauhusiano na mabadiliko ya tabia nchi?

Mtangazaji 2: Kabisa! Na misitu pia hutupatia dawa, chakula, na wanyama wa porini. Miti pia huchuja (filter) hewa yetu sayarini na kuhifadhi gesi chafu (CO_2) ili kupunguza ongezeko la kiwango cha joto duniani.

Mtangazaji 1: Lo! Basi kulinda misitu yetu ni jambo muhimu sana!

Mtangazaji 2: Ndiyo hivyo! Ninashangaa uhusiano wa watu wengine na misitu ni upi, na jinsi vijana wanaweza kushiriki katika harakati za kurejesha misitu na kupanda miti upya?

Mtangazaji 1: Nadhani hii ni nafasi nzuri ya kusikia kutoka kwa wasikilizaji wetu. Tungependa kusikia kutoka kwako. Je, vijana wenzako wanahusika vipi katika kupambana na ukataji wa miti? Unafikiri watu wanawezaje kujishirikisha au kuanzisha miradi yao wenyewe ya upandaji miti?

[TAJA ANAYEHOJIWA]
[CHEZA MAHOJIANO]
[SHIRIKISHA WASHIRIKI WAKO KWA KUULIZA MASWALI NA KUWAPA FURSA

MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kuunda kipindi chako.

YA KUTOA MAONI YAO WAZI WAZI]

Mtangazaji 1: Imekuwa vizuri kusikia kutoka kwa wasikilizaji wetu. Ikiwa sisi tunataka kubadilisha masuala yanayohusu ukosefu wa usawa na haki za mabadiliko ya tabia nchi (climate justice) katika jamii yetu kikamilifu, basi tunahitaji kukutana na kukuza uelewa wetu sote kila wakati! Ujumbe ni kwamba haki za mabadiliko ya tabia nchi inapaswa kuwa na mtazamo wa kuboresha haki za kijinsia, uchumi, nishati, rangi/kabila na mazingira katika jamii zetu pia. Zote zimeunganishwa! “

Mtangazaji 2: Ndio! Na inamaanisha kwamba wengi wetu tunaathiriwa na misitu na wanyama pori, hata ikiwa ni kwa kupitia bei ya vyakula au madawa.

Mtangazaji 1: Dah! Mazungumzo ya leo yamekuwa ya kuelimisha na kusisimua kabisa! Jiunge nasi wiki ijayo siku ya [TAJA SIKU na SAA ZA KIPINDI]. Tutazungumza kuhusu [TAJA MADA YA KIPINDI CHA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri!

MAANDALIZI YA KIPINDI CHA REDIO



MAADILI NA IDHINI

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao za kibinafsi.